# Maelekezo juu ya uunganishaji wa familia kwa mkimbizi aliyechaguliwa kupewa makazi mapya nchini Ufini

## Uombaji wa kibali cha makazi kwa msingi wa uhusiano wa kifamilia – muhtasari

### Nani ni mwanafamilia kwa mujibu wa sheria ya Ufini?



- mwanandoa au mwenza wa uhusiano uliosajiliwa
- mlezi wa mtoto aliye chini ya miaka 18
- mtoto aliye chini ya miaka 18 ambaye hajafunga ndoa.

### Nani siyo mwanafamilia kwa mujibu wa sheria ya Ufini?

- mtoto mwenye umri wa mtu mzima na wanafamilia wake
- wazazi wa mtu mwenye umri wa mtu mzima
- ndugu wa tumbo moja
- ndugu wengine.

### Jinsi gani mwanafamilia ataomba kibali cha makazi?




- kwa kuwasilisha ombi kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia huduma ya Enter Finland (www.enterfinland.fi), na baada ya kufanya hilo mwanafamilia anapaswa kuhudhuria ubalozi wa nchi ya Ufini AU
- kwa kuwasilisha ombi kwa njia ya karatasi, inayojazwa na mwanafamilia anayeishi nchi ya nje na kulipeleka mwenyewe kwenye ubalozi wa nchi ya Ufini.

### Kuomba kibali cha makazi ina bei gani?



- Bei ya ombi kwa njia ya kielektroni kwa mtu mzima ni 750 € na kwa mtoto 400 €.
- Bei ya ombi kwa njia ya karatasi kwa mtu mzima ni 800 € na kwa mtoto 430 €.

### Nini maana ya vigezo vya mapato?

- Utoaji wa kibali cha makazi una vigezo vyake, kwamba familia inaweza kujimudu na fedha zao nchini Ufini kuanzia mwanzoni. Wenye mamlaka wameainisha, fedha gani zinakuwa za kutosha kwa kuhakikisha uwezo wa familia kujikimu.
- Kama mwanafamilia wa mkimbizi aliyepewa makazi mapya anatoa ombi la kibali cha makazi ndani ya miezi mitatu, kuanzia wakati mwunganishaji wa familia alipopata taarifa juu ya kibali chake cha makazi, vigezo vya mapato havitakuwepo. Masharti yake ni kwamba familia imeundwa kabla ya mwunganishaji wa familia alipopata kibali chake cha makazi nchini Ufini. Anayeitwa mwunganishaji wa familia ni mwanafamilia anayeishi nchini Ufini.
- Vigezo vya mapato havitakuwepo, kama mwanafamilia anayeishi nchini Ufini ana umri mdogo na anayeishi Ufini bila mzazi au mlezi.

**Maelezo ya ziada juu ya uunganishaji wa familia yanapatikana kwenye kurasa zifuatazo.**

# Uombaji wa kibali cha makazi kwa msingi wa uhusiano wa kifamilia – maelezo ya ziada

## Mwanafamilia kwa mujibu wa sheria ya Ufini

Idara ya Uhamiaji inaamua juu ya utoaji wa kibali cha makazi kwa msingi wa uhusiano wa kifamilia kwa wanafamilia au ndugu wengine wa wakimbizi.

Dhana ya familia ya Kifini ni finyu kuliko ilivyo kwenye nchi nyingi. Wigo wa wanafamilia umeainishwa na sheria, na pengine hauendani na jinsi watu wanavyoelewa wanafamilia kwenye familia zao.

**Wanafamilia** ni watu wa familia ambao wako ndani ya familia inavyosemekana ni kama familia ya msingi, ambao ni

- mwanandoa au mwenza wa uhusiano uliosajiliwa
- mwenza bila ndoa kwa vigezo mahususi
- mlezi wa mtoto aliye chini ya miaka 18
- mtoto aliye chini ya miaka 18-vuotias ambaye hajafunga ndoa.

Kigezo kwa uunganishaji wa familia ya wanandoa na wenye mahusiano ya kimapenzi yaliyosajiliwa, ni kwamba wenza wote wawili wanapaswa kuwa na angalau miaka 21, wakati kibali cha makazi kinapoanza kufanya kazi. Kama wenza wana watoto wa kuzaa pamoja, mlezi wa mtoto anaweza kupewa kibali cha makazi, hata kama mlezi yuko chini ya miaka 21.

**Ndugu** wasio wanafamilia ni kwa mfano ndugu wafuatao:

- mzazi wa mtu mwenye umri wa mtu mzima
- ndugu wa tumbo moja wa mtu ambaye hajafunga ndoa au mtoto mwenye umri wa mtu mzima
- ndugu wa tumbo moja wa mtoto mwenye umri mdogo anayeishi nchi nyingine.

Watu ambao hawachukuliwi kama ndugu wengine kwa mtu anayeishi nchini Ufini ni kwa mfano wazazi au ndugu wengine wa mwenzake.

### Utoaji wa kibali cha makazi kwa mtu mwingine zaidi ya mwanafamilia wa familia ya msingi

Utoaji wa kibali cha makazi kwa msingi wa uhusiano wa kifamilia kwa mtu mwingine zaidi ya mwanafamilia wa familia ya msingi siyo ya kawaida kabisa na ni jambo la nadra. Utoaji wa kibali unaweza kufikiriwa, kama huyo ndugu anamtegea kabisa ndugu yake anayeishi nchini Ufini au kama wanadhamiria kuendelea na maisha thabiti ya kifamilia kama vile walivyokuwa kuishi zamani. Japokuwa, kibali cha makazi hakiwezi kutolewa kwa msingi pekee wa maisha ya kifamilia ya zamani. Yanayozingatiwa pia ni kwa mfano muda gani wahusika waliwahi kuishi pamoja, mawasiliano, uhusiano wa undugu, familia ya msingi, ndugu wa karibu walio kwenye nchi ya nyumbani pamoja na uwezo wa ndugu anayeishi nchini Ufini kuunga mkono kiuchumi kwa ndugu

yake. Kutokana na sababu za kiafya pekee kibali cha makazi hakitatolewa. Aidha desturi ya inchi ya kuwajibisha watoto kuwatunza wazazi wao waliozeeka siyo msingi kwa utaji wa kibali cha makazi  nchini Ufini. Ndugu fulani hana haki ya kuchagua, kwamba mtoto mwenye umri wa mtu mzima anayeishi nchini Ufini anapaswa kumtunza, bali inatosha mtu mwingine akiwa kumtunza.

## Uombaji wa kibali cha makazi kwa msingi wa uhusiano wa kifamilia

Mwanafamilia au ndugu mwingine atawasilisha ombi lake la kibali cha makazi kwa msingi wa uhusiano wa kifamilia au undugu mwenyewe kwenye ubalozi wa nchi Ufini uliopo nje ya nchi. Mwunganishaji wa familia anayeishi nchini Ufini hawezi kuwasilisha ombi kwa niaba ya mwanafamilia wake au ndugu mwingine.

Ombi linaweza kuwasilishwa kielektroniki pia kwa kutumia huduma ya mtandao ya Idara ya Uhamiaji iitwayo Enter Finland, kwenye anwani ya www.enterfinland.fi. Japo inabidi mwombaji (mwanafamilia au ndugu mwingine) afike kwenye ubalozi wa nchi ya Ufini kwa ajili ya kuthibitisha utambulisho wake na kutoa vitambulisho vya kibayometriki vinavyotakiwa na sheria, kama vile picha ya uso na alama za vidole. Mwombaji anapaswa kutembelea ubalozini ndani ya miezi mitatu baada ya kuwasilisha ombi. Mwombaji anatakiwa kuwa na ujuzi wa lugha wa kutosha na uwezo wa kutumia kompyuta kwa ajili ya kutumia ile huduma ya mtandao.

Ombi la kibali cha makazi hutozwa ada ya uchakataji. Mwaka 2026 kwa mtu mwenye umri wa mtu mzima ada ya uchakataji ya ombi kwa njia ya kielektroniki ni 750 € na kwa njia ya karatasi 400 €. Ada ya uchakataji ya ombi la mtu mwenye umri mdogo kwa njia ya kielektroniki ni 800 € na kwa njia ya karatasi 430 €.

Mwombaji anastahili kutoa ufafanuzi wa kutosha juu ya utambulisho wake na uhusiano wa undugu na mwanafamilia wake anayeishi nchini Ufini. Kimsingi nyaraka zilizohalalishwa zitahitajika. Mwombaji anapaswa kukaa kihalali kwenye nchi ambapo ombi la kibali cha makazi linafunguliwa.

## Kigezo kuhusiana na muda wa ukaaji

Kama familia imeundwa baada ya mwunganishaji wa familia amekubaliwa kuchaguliwa ndani ya kikomo cha nchi ya Ufini kuwapokea wakimbizi, mwunganishaji wa familia atakuwa na kigezo cha muda wa ukaaji. Inamaanisha, kwamba inabidi mwunganishaji wa familia awe ameishi nchini Ufini angalau miaka miwili kwa kibali cha makazi, kabla ya mwanafamilia au ndugu mwingine kuweza kuomba kibali cha makazi cha Ufini kwa msingi wa uhusiano wa kifamilia. Muda wa ukaaji wa miaka miwili unahesabika kuanzia ile siku mwunganishaji wa familia alipohamia nchini Ufini. Kigezo kuhusiana na muda wa ukaaji kinaweza kutozingatiwa katika baadhi ya kesi, kama kuna sababu nzito isiyo kawaida, au ni lazima kwa manufaa ya mtoto.

## Vigezo vya mapato

Utoaji wa kibali cha makazi una vigezo, kwamba familia inayoishi nchini Ufini inapaswa kuwa na uhakika wa mapato ya kujikimu ambayo siyo mafao yanayolipwa na mashirika ya kijamii. Mapato yenye uhakika wa kujikimu humaanisha, kwamba familia inapaswa kuwa na uwezo wa kifedha wa kutosha kuishi nchini Ufini. Uwezo wa kifedha unaohitajika umeainishwa na wenye mamlaka, na hutegemea kulingana na ukubwa wa familia. Maelezo ya ziada kuhusu vigezo vya mapato: www.migri.fi/toimeentuloedellytys-kansainvalista-suojelua-saaneen-perheenjasenelle.

Wanafamilia wa mkimbizi aliyepewa makazi mapya wanaweza kuomba kibali cha makazi bila vigezo vya mapato kwa muda wa miezi mitatu, kama familia imeundwa kabla ya mwunganishaji wa familia alipokubaliwa kuchaguliwa ndani ya kikomo cha nchi ya Ufini kuwapokea wakimbizi. Muda wa miezi mitatu uliowekwa unaanza wakati mwunganishaji wa familia akiwa amepata taarifa juu ya kubaliwa kuchaguliwa ndani ya kikomo cha kuwapokea wakimbizi. Wanafamilia wanaweza kuomba kibali cha makazi hata baada ya muda wa miezi mitatu uliowekwa, lakini baada ya kipindi hicho kupita, kuna vigezo kwamba mapato yao ya kujikimu nchini Ufini yana uhakika. Vigezo vya mapato havitakuwepo, kama mkimbizi anayeishi nchini Ufini ana umri mdogo.

Mapato ya ndugu wengine ya kujikimu yanapaswa kuwa na uhakika wakiwa wanaomba kibali cha makazi kwa msingi wa uhusiano wa kifamilia.